

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Simu Nambari: 2152532/3

Fax Na: 2152820

(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe
kwa Kamishna Jeneral)



8 Barabara ya Kivukoni,
S. L. P. 80327,
11486 DAR ES SALAAM.

TAARIFA KWA UMMA

SERIKALI HAIJARUHUSU KILIMO CHA BANGI

Dar es Salaam, 28 Mei, 2021:

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) inautaarifu Umma kuwa, mpaka sasa Serikali haijaruhusu kilimo cha zao la bangi Nchini. Hii ni kutokana na madhara mbalimbali yanayotokana na matumizi ya dawa hiyo ya kulevya.

Ikumbukwe kuwa, taarifa inayosambaa ikieleza kuwa Umoja wa Mataifa umeruhusu kilimo cha bangi kwa matumizi ya binadamu siyo sahihi, isipokuwa Umoja huo umerekebisha baadhi ya vipengele vya udhibiti wa bangi pamoja na mazao yake ili nchi nyingi ziweze kuridhia bangi itumike katika tafiti na kutengeneza dawa za tiba. Aidha, taarifa hiyo ya Umoja wa Mataifa inasisitiza kuwa, **bangi itaendelea kuwa dawa ya kulevya inayodhibitiwa Kimataifa.**

Kwa muktadha huo, Mamlaka inawaomba wananchi kupuza taarifa zinazohamasisha uhalalishaji wa kilimo na matumizi ya dawa za kulevya aina ya bangi Nchini. Vilevile inatoa wito kwa wananchi na jamii kwa ujumla kuendelea kushiriki katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya kwa kutoa taarifa juu ya watu wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Imetolewa na,

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Florence Khambi".

Florence Khambi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.